

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**TAARIFA YA WAGONJWA WALIOTHIBITIKA KUWA NA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA KATIKA MAABARA KUU YA TAIFA, TAREHE 30 MACHI 2020**

Ndugu Wananchi,

Ninapenda kutoa taarifa kwamba leo 30 Machi 2020 tumethibitisha kuwepo kwa wagonjwa wapya watano (5) wa COVID-19 baada ya kufanyiwa vipimo katika Maabara yetu Kuu ya Taifa. Kati ya wagonjwa hawa, watatu (3) ni kutoka Dar es Salaam na wawili (2) kutoka Zanzibar, ambao taarifa zao zitatolewa na Waziri wa Afya Zanzibar.

Hivyo sasa jumla ya wagonjwa wa COVID-19 nchini ni kumi na tisa (19) akiwemo mgonjwa mmoja aliyetolewa taarifa na Waziri wa Afya wa Zanzibar tarehe 28/03/2020.

Taarifa za wagonjwa wapya wa Dar es salaam ni kama ifuatavyo:

1. Mwanaume, mwenye umri wa miaka 49, mtanzania alikutana na raia wa kigeni kutoka miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi,
2. Mwanamke, mwenye umri wa miaka 21, mtanzania ambae ni miongoni mwa watu waliokuwa wakifuatiliwa,
3. Mwanaume, mwenye umri wa miaka 49, mtanzania ambae pia ni miongoni mwa watu waliokuwa wakifuatiliwa,

Kazi ya kufuatilia watu wote wa karibu waliokutana na wagonjwa hawa inaendelea (contact tracing). Aidha tunawataka wananchi wote kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na ugonjwa huu.

A handwritten signature in green ink, appearing to read 'Umyy A Mwalimu'.

**Umyy A Mwalimu (Mb)**

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**  
**30 Machi 2020**